# OFISI YA RAIS

# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# WILAYA YA KILOLO KISWAHILI

## MTIHANI WA MUUNGANO

## KIDATO CHA NNE

**MUDA: SAA 3:00** **APRILI, 2025**

---

**MAELEKEZO**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali kumi na moja(11)
2. Jibu maswali yote katika sehemu A, B na maswali mawili (2) katika sehemu C swali la tisa (09) ni la lazima
3. Sehemu A ina alama kumi na sita (16), sehemu B ina alama hamsini na nne (54) na sehemu C ina alama thelathini (30)
4. Zingatia maelekezo ya kila sehemu na ya kila swali
5. Andika namba yako ya mtihani katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

**SEHEMU A (Alama 10)**

**Jibu maswali yote katika sehemu hii**

1. Katika kipengele (i) – (x), chagua jibu sahihi kisha andika herufi ya jibu hilo kwenye kijitabu chako cha kujibia.

(i) Kimapokeo, nomino inayojitokeza upande wa kiarifu inaitwa…………….

A. Kiima
B. Chagizo
C. Shamirisho
D. Kiarifu
E. Prediketa

(ii) Neno thamani lina herufi ngapi?

A. Tatu
B. Sita
C. Saba
D. Nne
E. Nane

(iii) Kiimbo hufasiliwaje katika mazungumzo?

A. Kuzungumza na kuongea kwa sauti
B. Kuzungumza na kupandisha sauti
C. Kuzungumza na kushusha sauti
D. Kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti
E. Kuimba na kupandisha sauti

(iv) "Sitaki, sitaki nasema sitaki kabisa kusikia" katika lugha ya kisanii sentensi hii ina…………

A. Sitiari
B. Takriri
C. Tashibiha
D. Tashihisi
E. Mubadagha

(v) Fasihi ni moja wapo ya kazi za Sanaa inayotumia __________ katika uwasilishaji wake

A. Fani na maudhui
B. Akili
C. Lugha
D. Maneno
E. Mitindo

(vi) Rais Samia hupenda sana kutumia methali na nahau katika hotuba mbalimbali, seti zifuatazo ni methali isipokuwa moja ni nahau je ni ipi?

A. Asiye na mwana aeleke jiwe
B. Aliye juu mngoje chini
C. Amemranda mama yake
D. Aliye mbali haangukiwi na mti
E. Asiye na hili na lile

(vii) Kategoria ya kisarufi inayowakilisha wakati katika kitenzi
A. Leksimu
B. Njeo
C. Kiambishi awali
D. Shina
E. Timilifu

(viii) Mende anapenda kula uchafu. Neno liliopigiwa mstari lipo katika ngeli ipi?
A. KI – VI
B. U – I
C. A – WA
D. KU
E. LI – YA

(ix) Sentensi zinazoelezea wazo moja ni
A. Aya
B. Insha
C. Kifungu cha habari
D. Kituo
E. Barua

(x) _____________ mawazo makuu ya mtunzi kuhusu maisha
A. Dhamira
B. Ujumbe
C. Falsafa
D. Mafunzo
E. Migogoro

2. Oanisha maana ya dhana zilizopo katika orodha A kwa kuchagua herufi ya dhana husika katika orodha B, kisha andika herufi katika karatasi yako ya kujibia.

| **ORODHA A** | **ORODHA B** |
|---|---|
| (i) Kaskazini mwa Msumbiji | A. Kishela |
| (ii) Kisiwa cha lamu | B. Kingwana |
| (iii) Kusini mwa Somalia | C. Kimwani |
| (iv) Mpakani mwa Kenya na Tanzania | D. Kimiini |
| (v) Kisiwa cha Tumbatu | E. Kivumba |
| (vi) Pwani ya kusini mwa Tanzania | F. Kimgao |
| | G. Kimatondoni |
| | H. Kitumbatu |

**SEHEMU B (Alama 54)**

**Jibu maswali yote katika sehemu hii**

3. (a) Nini maana ya masamiati
   (b) Taja na kisha ueleze kwa kifupi njia zinazotumika kuunda msamiati wa Kiswahili sanifu.tumia hoja (05) tano.
   (c) Ni mambo gani yanayopelekea kuundwa kwa msamiati? Tumia hoja (03) tatu.

4. Kwa niaba ya wanafunzi wenzako andika risala kwa Mkuu wa shule yako ukimweleza mikakati yenu kimasomo na kimaisha na namna ya kukabiliana na changamoto zinazowakabili.

5. (a) Huku ukitoa mifano toa maana ya dhana zifuatazo
   (i) Ngeli za Nomino
   (ii) Upatanisho wa kisarufi
   (iii) Orejeshi

   (b)Huku ukitoa mifano taja dhima za o – rejeshi. Eleza hoja (3) tatu

6. Ni mambo gani yaliyochangia na yanaendelea kuchangia kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili baada ya uhuru.  Hoja sita (6)

7. Kwa kutumia Riwaya ya watoto wa mama Ntilie onesha mchango chanya wa mwanamke katika Maendeleo. Hoja (6)

8. Usimulizi wa hadithi hufanyika kwa kutumia mbinu mbalimbali za kisanaa ambazo hufanya usimulizi huo uwe na mvuto kwa hadhira (taja mbinu hizo 6)

**SEHEMU C (Alama 30)**

Jibu maswali mawili tu (**2**) kutoka katika sehemu hii. Swali la tisa (**9**) ni lazima.

**ORODHA YA VITABU**

**USHAIRI**
Wasakatonge -M.S. Khatibu (DUP)
Malenga wapya -TAKILUKI (DUP)

| | |
|---|---|
| Mashairi ya chekacheka | -T.A Mvungi (EP/D.LTD) |
| **RIWAYA** | |
| Takadini | -Ben J. Hanson (MBS) |
| Watoto wa mama ntilie | -E. Mbogo (H.P) |
| Joka la mdimu | -A.J Safari (H.P) |
| **TAMTHILIYA** | |
| Orodha | -Steve Reynolds (MA) |
| Ngoswe penzi kitovu cha uzembe | - E.Semzaba (ESC) |
| Kilio chetu | -Medical Aid Foundation (TPH) |

9. Lugha anayoitumia mwandishi katika kazi yake ya fasihi ndiyo inayosaidia katika kufikisha wazo lake kwa hadhira. Kwa kutumia riwaya teule mbili (02) ulizozisoma onesha jinsi wasanii wa riwaya hizo walivyotumia kipengele cha tamathali za semi.

10. "Kufuatana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia nafasi ya fasihi andishi katika Tanzania ya sasa haina umuhimu sana" Jadili kauli hiyo kwa kutumia vitabu viwili vya ushairi vilivyoorodheshwa.

11. Eleza ni kwa namna gani mwandishi amefeli na kufaulu katika kipengele cha fani na maudhui. Kwa kutumia tamthiliya mbili ulizozisoma eleza dai hilo kwa kutoa hoja tatu kila kitabu.